# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuichangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae tuipitishe bajeti iliyopo mbele yetu kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa masikitiko makubwa, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ilipokea taarifa ya msiba wa Rais mstaafu wa awamu ya pili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais mstaafu wa awamu ya tatu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Alhajj Ali Hassan Mwinyi. Msiba huo umeacha pengo kubwa kwa familia na Taifa kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu mtukufu amweke mahali pema marehemu na awape subira viongozi wetu na familia yake, Amiin.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake imara na nia yake ya dhati ya kukuza uchumi wa nchi hii kupitia sekta ya uwekezaji, ambapo kwa kipindi cha uongozi wake jumla ya miswada minne (4) imepitishwa na kusainiwa kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa shukurani za dhati kwa vingozi wakuu wa nchi yetu ambao ni Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kushauriana vyema na Mheshimiwa Rais kwenye masuala mbali mbali ya uendeshaji wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nitumiye nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mheshimiwa Shariff Ali Sharifu kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii ambayo imebeba sekta muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Aidha, Kamati inatoa shukurani kwa Makatibu wakuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili mafungu ya bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na muundo wake, Wizara hii inasimamia mafungu matatu 03 ya bajeti. Kamati yangu ilipata fursa ya kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji), fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) na fungu A11 (Wakala wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi) siku ya Jumanne tarehe 07 Mei, 2024 na kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo pamoja na marekebisho madogo iliyoyapendekeza.

Wajumbe wa Kamati ya Utalii Biashara na Kilimo walifanya kazi kubwa ya kuyapitia kwa kina mafungu hayo ya bajeti ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina Wajumbe hao pamoja na Makatibu wao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
10. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
11. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
12. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo Wizara kupitia fungu A07 inakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 6,695,428,000 ambazo ni ongezeko la asilimia 41 ya makadirio ya mwaka 2023/2024.

Fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu A07 linaloshughulikia Kazi na Uwezeshaji linakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. Bilioni 6,695,428,000 ambayo ni ongezeko la asilimia 41 kutoka makadirio ya makusanyo ya mwaka 2023/2024. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo muhimu na inaiomba kuhakikisha mapato hayo yanakusanywa kwa asilimia mia moja na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

Aidha, fungu A07 linakadiriwa kutumia jumla ya Tzs. bilioni 7,273,300,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ujumla, programu hii inakadiriwa kupatiwa jumla ya Tsh. bilioni 2,178,000,000 kwa kazi za kawaida ambayo ni ongezeko la asilimia 25 ya makadirio ya mwaka uliopita. Hatua hii ni muhimu kwa uratibu na uendelezaji wa ajira kwa vijana pamoja na usimamizi wa usalama na afya kazini.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Milioni 247,020,000 kwa ajili ya uimarishaji wa mfumo wa ukaguzi wa usalama na afya kazini. Mfumo huo una umuhimu mkubwa kwa Wizara na Taifa kwa ujumla kwani utapelekea shughuli za ukaguzi wa usalama na afya kazini kufanyika kwa wepesi na kuimarisha mazingira bora kwa wafanyakazi wa umma na sekta binafsi pamoja na kulinda afya zao.

Aidha, Kamati imebaini kuwa Idara ya Usalama na afya kazini inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vifaa na watendaji unaopelekea kushindwa kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Hadi sasa Idara imefanikiwa kufanya kaguzi za usalama kazini tu na kushindwa kulifanyia kazi suala la afya kazini ambapo hulazimika kutafuta wataalamu wa nje ya Wizara kwa ajili ya shughuli hiyo na kukosa mapato yanayolipwa katika eneo hilo. Hivyo, Kamati inashauri Idara hii iimarishwe kwa kupatiwa nyenzo na wataalamu wa kutosha ili kulinda afya za wafanyakazi na kuwajengea ari ya kiutendaji.

## PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefarajika na nyongeza ya fedha zilizokadiriwa kwa Programu ndogo ya **Usimamizi na Uimarishaji wa vyama vya ushirika.** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu ndogo hii inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 1,080,725,000 ambayo ni ongezeko la asilimia 24 ya mwaka uliopita. Upatikanaji wa fedha

hizo utasaidia kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika na kuvilea hadi kufikia katika maendeleo makubwa na kujikwamua kutokana na umasikini. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kusimamia kikamilifu matumizi ya programu ndogo hii kwa maslahi ya Taifa.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kutenga fedha zaidi kwa programu ya uendeshaji na uratibu wa Afisi ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya Tzs. 4,014,575,000. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara kuzitumia vyema fedha hizo kwa maslahi ya Watendaji na kuleta tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu A08 linaloshughulikia Uchumi na Uwekezaji linakadiriwa kutumia jumla ya Tzs. Bilioni 21,053,100,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Tunaipongeza Wizara kwa kutenga fungu hilo ili kuziwezesha shughuli za Uchumi na Uwekezaji kufanyika kwa ufanisi.

**PROGRAMU KUU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA**

MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi Kupitia Uwekezaji inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. bilioni 18,645,800,000. Fedha hizo ni ongezeko la asilimia 192 ya makadirio ya programu hii ndogo kwa mwaka uliopita ambayo ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 6,387,800,000. Kamati yetu imeridhishwa na hatua hii ambayo inakwenda sambamba na utekelezaji wa sera ya Uwekezaji ambayo ndiyo chachu ya maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imefarajika na suala la kutengwa jumla ya Tzs. 24,000,000. ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ambalo litakuwa na haiba inayolingana na dhima ya Taasisi hiyo kwa uchumi wa nchi hii. Ni matarajio ya Kamati yetu kuwa, taratibu za ujenzi wa jengo hilo zitakamilika ndani ya wakati uliopangwa na kuifanya ZIPA kutoa huduma bora zaidi kwani mazingira bora yana mchango mkubwa katika utoaji wa huduma bora kwa jamii.

**Fungu A11(Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inatoa pongezi za dhati kwa Serikali, kupitia Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kuipatia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi fungu maalum la bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati iliyapitia

matumizi ya fungu hilo kwa kazi za kawaida na shughuli za maendeleo na kushauri mambo mbalimbali.

**PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu A11 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) linakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. bilioni 46,879,700,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo, jumla ya Tsh. 3,279,700,000 ni kwa kazi za kawaida na Tsh. 43,600,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Huduma ya kutoa na kuratibu mikopo yenye masharti nafuu (HA11010101) inakadiriwa kutumia asilimia 89 ya jumla ya fungu zima. Kamati yetu imefarajika sana kwa kuelekezwa fedha nyingi kwenye huduma hii na inashauri Wakala kuzitumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watumie fursa hii kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale waliyojipangia kwa ufanisi.

**MheshimiwaS pika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati yangu naiunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

……………………

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf,
Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**